

LAIKIPIA



UNIVERSITY

## UNIVERSITY EXAMINATIONS

1<sup>ST</sup> SEMESTER 2025/2026 ACADEMIC YEAR

### THIRD YEAR EXAMINATIONS FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF ARTS KISWAHILI AND COMMUNICATION

**KICO 312: FASIHI ANDISHI NA MAWASILIANO**

***STREAM: R***

***TIME: 2 HRS***

***DAY: TUESDAY (2.30-4.30PM)***

***DATE: 27/1/2026***

**THIS QUESTION PAPER CONSISTS OF THREE (3 PAGES)**

**PLEASE DO NOT OPEN UNTIL THE INVIGILATOR SAYS SO.**

**MAAGIZO:**

1. Jibu maswali **MATATU PEKEE. SWALI LA KWANZA** ni la lazima na **MASWALI YOYOTE MAWILI** kati ya manne yaliyosalia.
2. Hakikisha umeandika nambari yako ya usajili kwenye kila ukurasa.

**SWALI LA 1 (LAZIMA) – (Alama 30)**

- (a) Eleza dhana ya fasihi andishi. **(alama 2)**
- (b) Fafanua uhusiano uliopo kati ya fasihi andishi na mawasiliano ya kijamii. **(alama 8)**
- (c) Tathmini historia ya fasihi andishi ya Kiswahili, ukionyesha hatua kuu tatu za maendeleo yake tangu enzi za utenzi hadi fasihi ya kisasa. **(alama 14)**
- (d) Eleza mchango wa fasihi ya watoto katika kukuza maadili na mawasiliano ya kijamii. **(alama 6)**

**SWALI LA 2 – (Alama 20)**

- (a) Eleza mchango wa utenzi katika kukuza na kuendeleza fasihi andishi ya Kiswahili. **(alama 8)**
- (b) Jadili mabadiliko ya mashairi ya Kiswahili kutoka mashairi ya kimapokeo hadi ya kisasa. **(alama 8)**
- (c) Kwa maoni yako, ni kwa namna gani mashairi ya Kiswahili yanachangia mawasiliano ya kijamii? **(alama 4)**

**SWALI LA 3 – (Alama 20)**

- (a) Tofautisha kati ya riwaya ya kijamii na riwaya ya kifalsafa, ukitumia mifano halisi. **(alama 8)**
- (b) Eleza jinsi mwandishi wa riwaya anavyoweza kutumia kazi yake kuibua mijadala ya kisiasa na kijamii. **(alama 6)**
- (c) Jadili umuhimu wa lugha katika kufanikisha mawasiliano ndani ya riwaya. **(alama 6)**

**SWALI LA 4 – (Alama 20)**

- (a) Onyesha tofauti **tatu** kuu kati ya tamthilia na hadithi fupi kama tanzu za fasihi andishi. **(alama 6)**

- (b) Kwa kutumia mfano wa tamthilia yoyote ya Kiswahili, eleza jinsi tamthilia inavyotumika kuikosoa jamii. **(alama 8)**
- (c) Eleza nafasi ya hadithi fupi katika kuhamasisha mabadiliko ya kijamii. **(alama 6)**

**SWALI LA 5 – (Alama 20)**

- a) Eleza kwa mifano mitatu jinsi fasihi andishi inavyotumika kama kioo cha jamii. **(6 alama)**
- b) Jadili dhima nne kuu za fasihi andishi katika jamii. **(alama 8)**
- c) Tathmini masuala ibuka yanayoathiri fasihi andishi ya Kiswahili katika karne ya 21, ukizingatia maendeleo ya kidijitali na utandawazi. **(alama 6)**

**MWISHO WA MTIHANI**